

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na CHB.148/S0S/01/11

23 Mei, 2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imepokea kibali cha utekelezaji wa Ikama na Bajeti kwa Ajira Mpya katika Mwaka wa fedha 2021/2022 yenye Kumb. Na. FA.97/228/01/9 cha tarehe 13/05/2022 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hivyo Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni amewatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoordheshwa hapa chini.

### **1.0 KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III - (NAFASI 4)**

#### **1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha IV waliohudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za **Windows, Microsoft Office, Internet, E-Mail na Publisher.**

#### **1.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- ii) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- iii) Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

- iv) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- v) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- vi) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisi walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- vii) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

**Mshahara:**

- i) Malipo ya Mshahara yatazingatia Ngazi ya Mshahara ya Serikali yaani **TGS B kwa Mwezi.**

**2.0 DEREVA DARAJA LA II - (NAFASI 2)**

**2.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Kuajiriwa kwenye Cheti cha Kidato cha NNE (Form IV) na Leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua Mwaka bila kusababisha ajali.
- ii. Awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- iii. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

**2.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- vi) Kufanya usafi wa gari, na
- vii) Kufanya kazi nyingine kadri anavyoelekeza na Msimamizi wake

**Mshahara: Malipo ya Mshahara**

- i) Malipo ya Mshahara yatazingatia Ngazi ya Mshahara ya Serikali yaani **TGS B kwa Mwezi.**

### 3.0 MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
- iii. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni
- iv. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- vi. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 06 Juni , 2022.
- x. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili hayatafikiriwa
- xi. Maombi yawasilishwe Kwa njia ya barua posta kwa:  
Mkurugenzi wa Manispaa,  
Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni,  
S.L.P 31902,  
KINONDONI.



Hanifa Suleiman Hamza  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**